**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**2 Augusti 2008**

**Waliohudhuria**
Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Aseli Wilison
Athmani Mussa
Dominata Rwechungura
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
Fredy H Lwila
George Kabogo
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Juma Imori Rugole
Jumanne Idd Selemani
Kibwana Mohammad Msiga
Musa Athumani Lahi
Mussa Alex
Mussa Saidi
Paulo Atibu Hatibu
Pendo Jaiueing
Ramadhani Rajabu Nyengo
Shukuru Hassan
Sosthenes C Amlima

**Mgeni**: Stephen Vincent, Global Transport Knowledge Partnership (gTKP)

**Stephen wa gTKP kututembelea**
UWABA tunapata email mara kwa mara kutoka gTKP (Global Transport Knowledge Partnership – shirika la taarifa ya usafiri duniani) na hii ni jinsi tumewasiliana na Stephen ambaye anashughulika na utawala wa serekali kwenye mambo ya usafiri. Alikuwa akitembelea Afrika Mashiriki na aliamua kuhudhuria mkutano wa UWABA.

Alieleza kuhusu kazi ya gTKP kwa kusaidia watu wa nchi mbali mbali kubadalisha mawazo kuhusu masuala ya usafiri. Alieleza kwamba gTKP inafanya kazi mbali mbali na kazi moja ambayo yeye anashughulika nayo ni kuangalia mambo ya utawala wa serekali na vipi serekali inasvyoshirikiana na mashirika ya siyo ya kiserekali. Amependa sana kusoma kwenye website yetu kuhusu uzoefu wa UWABA kuwasiliana na serekali. Alipendekeza tuandika repoti pamoja kuhusu uzeofu wetu isomeke kwenye mkutano kuhusu mambo ya usafiri wa Afrika Cameroon mwezi wa Septemba, na pia labda mwanachama wa UWABA ataweza kuhudhuria mkutano pia.

Tuliuliza kuhusu masuala ya lugha kwenye mkutano Cameroon na alisema ingekuwa nzuri kuwa na mwanachama wa UWABA ambaye anaweza kuwasiliana sana kwa kiingereza kwa sababu mkutano utakuwa kwa kiingereza na kifaranza. Pamoja tulipata wazo la mkutano wa Afrika Mashiriki ambapo Kiswahili kitakuwa lugha moja ya mkutano, ambapo wanachama wengi zaidi wa UWABA wanaweza kushirikiana. Stephen alisema atapenda kutayarisha mkutano kama huu.

Wanachama mbali mbali wa UWABA tulimshukuru Stephen kwa kututembelea na kuhudhuria mkutano wetu. Tulieleza kidogo kuhusu uzoefu wetu wa kuwasiliana na serekali yetu pamoja na donors kama umoja wa Ulaya. Dominata aliongea kuhusu umuhimu wa elimu na msaada wa elimu kuhusu mambo ya usafiri kutoka shirika la like gTKP ilituwasiliane vizuri zaidi na serekali.

**Wanachama wapya**
Wamachama wapya Mussa Saidi, George Kabogo, Fredy Lwila na Athmani Mussa walijitambulisha na tuliwakarabisha kwenye UWABA.

**Ofisi**
Hii ilikuwa mkutano wetu wa kwanza kwenye ofisi yetu mpya Manzese Sisi kwa Sisi. Jumatatu Aseli, Filbert na Juma walihamisha bao za tangazo na rafu na waliziweka kwenye ofisi mpya. Rafiki mmoja wa Mejah alichora kwa penceli lakini bado hajapaka rangi kabisa – Mejah alituma ujumbe kuomba samahani kazi hii haijakamilika bado. Jumanne alisema atawaeleza mtu yeyote anayefika ofisi ya zamani vipi kufika ofisi mpya.

Ally Saidi Mohammed alitumia ujumbe kwa kupita Jumanne kwamba anaweza kutengeneza bao nyeusi kwa Tsh 49,000 lakini hajasema ya saizi gani. Amar alitumia email kwamba bao nyeusi ya 120cm x 180cm ni Tsh 54,000 na bao nyeupe ya 60cm x 90cm ni Tsh 36,000. Tulikubali kutafuta bao nyuesi kwa sababu bao nyeupe inatakiwa marker pens ambazo ni za bei ghali. Shukuru alisema ameona bao nyeusi ndogo kwa Tsh 40,000 mpaka Tsh 50,000. Tlikubali kusubiri mpaka wiki ijayo kufanya uamuzi kwa sababu Ally Saidi Mohammed na Amar watakuwepo.

**Mradi wa usalama barabarani - Wamba Memorial Fund**
Elaine alichapa mawazo yote ambayo washirika waliandika wakati wa mafunzo na aliziweka katika faili ya Wamba Memorial Fund. Pia aliweka repoti ya Andrew's kwenye faili. Tulikubali kupata bao nyeusi kabla ya kuanza kufundishana.

**Mkutano wa kila mwezi kuhusu masuala ya baisikeli**
Andrew alisema kwa email kwamba ataweza kuandika barua kupendekeza serekali ianzisha mkutano wa kila mwezi kuhusu mambo ya baisikeli ya Dar es Salaam na Elaine alikubali kwamba hii itakuwa mchango mzuri. Edgar alisema tuwaandikie hiyo barua kwa watu wa manispaa pia..

**Rais Kikwete**
Dominata alitafuta taarifa wakati wa wiki kwamba Rais alitoa hotuba Tanga, Uwanja wa Mkwakwani kuhamasisha watu wa Tanga kuendelea kutumia baiskeli kwa sababu ya kupanda bei ya mafuta, na hotuba ilikuwa kwenye East Africa Radio.

Sosthenes alipendekeza tuombe kaseti kutoka TBC na Paulo alisema atafuatalia.

Elaine ataandika barua kwa Rais na kuleta kwenye mkutano wa wiki ijayo ili wanachama wapitie.

**Msafara wa baiskeli**
Elaine alileta proposal ya mwaka huu ya msafara wa baiskeli kwenye mkutano. Sosthenes alipendekeza tuongeze fulana / t-shirt kwenye orodha ya aina ya udhamini tuanyotafuta. Tulikubali kuandika barua kwanza kwa mashirika ambao walitudhamini mwaka jana.

**Documentary**
Amar alisema kwa email kwamba atapenda kufanya documentary ya TV kuhusu UWABA na masuala ya baiskeli Dar es Salaam. Wanachama walisema hii itasaidia sana. Elaine alipendekeza Amar aongeze katika kazi hii na ashirikiane na Sosthenes na Mejah.

**Kupiga round kila wiki**
Tulikubali kwamba kuanzia wiki ijayo tutaendesha baiskeli pamoja maeneo ya Manzese ili kujitangaze.

**Vipeperushi**
Juma alitembelea kampuni ya guta na walipenda sana ufuataliaji wa UWABA kuhusu mambo ya kodi na mambo mengine. Walichangia kufanya photocopy 800 ya vipeperushi tuliyosambaza kwenye msafara wa baiskeli mwaka jana. Wanachama walimpongeza Juma kwa kupata mchango huu kwa ajili ya UWABA. Anwani kwenye barua ni anwani ya Mabibo basi tulikubali kila mtu aje na kalamu kwenye mkutano wa wiki ijayo na turekebishe pamoja.

**Posho ya Juma**
Elaine aliongea kuhusu kazi kubwa Juma anafanya kwa ajili ya UWABA, ambayo ni nyingi sana kuliko kujitolewa kwa kawaida na anatumia muda wake mwingi kila wiki. Alipendelea UWABA tuanzishe tena taratibu ya kumpa posho ya kila mwezi ya Tsh 20,000 ambayo tulianzisha halafu tuliisimamisha tena. Wanachama waliongea na walikubali kuanzisha tena utaratibu huu. Jumanne alipendekeza kila mtu asaini karatasi kuonyesha kwamba wanakubali na hiyo na wote walifanya hivyo.

**Baisikeli ya Kibwana**
Hussein Hamza alikagua baisikeli ya walemavu ya Kibwana na alikuwa na mapendekezo kuhusu marekebisho lakini hakuweza kuhudhuria mkutano kwa sababu ya msiba basi ataeleza wiki ijayo.

**Mambo ya hela**
Elaine na Juma walikaa pamoja jumapili na waliandika mahesabu ya mafuzo ya wakufunzi, lakini Elaine alisahau kuileta kwenye mkutano – ataleta wiki ijayo. Waliona hela ya UWABA ambayo Elaine anabaki nayo ni Tsh 155,000 basi wakati wa wiki alirudisha hela hii kwenye akaunti ya UWABA.

Tairi mypa mbili kwa ajili ya guta la UWABA zilitakiwa na Juma alizinunua wakati wa wiki kwa Tsh 52,000.

Pia wakati wa wiki Juma alitumia Tsh 400 kusafiri na ferry kutana na Elaine, Tsh 11,500 kwa ajili ya nyororo mpya na sahani mpya ya baisikeli yake anayotumia kwa ajili ya kazi ya UWABA, Tsh 2,000 kwa simu na Tsh 750 kwa misumari ya ofisi.